Desemba 27, 2015
Mr Nicos Anastasiades,
Rais wa Jamhuri ya Cyprus,
Jamhuri ya Cyprus,
Nikosia.

Nakuandikia barua hii kama dharura kufuatia maamuzi ya ajabu na yenye kuharibu yaliyofanywa na Benki Kuu ya Cyprus (CBC), na taarifa kupelekwa FBME tarehe 21 Desemba, kufuta leseni ya tawi la Cyprus la FBME. Hii inafuatia miezi 17 ya CBC kuliongoza vibaya tawi hilo, kipindi ambacho ilisababisha kitengo tanzu cha kadi cha FBME kufungwa na wafanyakazi wake takriban 80 kupunguzwa kazi na kuwanyima wateja uhuru wa kutumia akaunti zao. Sasa, maisha ya zaidi ya wafanyakazi 250 wa Benki ya FBME nchini Cyprus yapo hatarini wakati CBC inaendelea na jitihada zake za kuizika Benki. Hii inafuatia uzembe ulioonyeshwa na CBC kwa vitendo vyake kwenye mabenki matatu ya Cyprus, yaliyokuwa chini ya usimamizi na kanuni zake.

Tuna wajibu wa kujitetea wenyewe baada ya kujaribu mbinu mbalimbali ili kuepusha balaa hili. Kufuatia barua yetu ya wazi kwako kutoka kwa mwanasheria wetu, Bw Alecos Markides, tunaelewa kwamba umeamua kutojihusisha kwenye jambo hili, Ingawaje sababu za kufanya hivyo hatujazijua bado. Tunaamini kwamba kuna kikundi kidogo cha maafisa wa CBC wamamekula njama na watu wengine wa nje, na kuitoa kafara FBME kwa idara ya Serikali ya Marekani bila sababu yoyote. Taarifa za awali za shutuma za CBC dhidi ya FBME zinazoonyesha njama hizo, zinathibitishwa kwenye kauli ya MOKAS ya 28 Julai 2014. CBC ilifanya tukio hili kuwa siri bila kuitaarifu FBME. Kafara ya FBME, inayopingwa kwa viwango vyote vya kimaadili, inaaminika imefanywa ili kuyalinda mabenki ya Cyprus na mapungufu ya CBC yenyewe.

Kwa sasa ni wazi kwamba CBC wanalazimisha makosa kwa upande wa FBME ili watengeneze ushahidi. Lakini, CBC inakabiliwa na kesi za kisheria zilizifunguliwa Washington na Paris, ambazo zote zinaonyesha FBME itashinda, kwa hiyo maofisa waandamizi wa CBC wana wasiwasi na madhara yatakayowakumba. Tunatoa wito kwako kama Rais wa Jamhuri ya Cyprus kuingilia kati kwa haraka na kufanya uamuzi kwa jambo hili na kuepusha madhara makubwa kwa nchi, kwa CBC na kwa FBME.

**Tatizo Lililopo Sasa**

Hatua ya CBC ya kuliweka tawi la FBME nchini Cyprus chini ya Azimio inapaswa kupingwa kisheria na Benki, kwa sababu haina mashiko ya kisheria. Huenda ukawa unafahamu kwamba vigezo vinavyotakiwa nchini Cyprus kwa sheria ya Azimio havikuwepo wakati CBC inafanya uamuzi wa pupa wa kuchukua milki ya tawi.

CBC ilishindwa kufikiria njia mbadala za kuaminika na uuzaji wa tawi, na walikataa kushauriana na ama mdhibiti mkuu wa FBME nchini Tanzania au Wanahisa wa Benki , bodi yake au uongozi kabla ya kuchukua uamuzi wake wa kibabe (na Benki ilikuwa na ukwasi wa kutosha kama inavyoendelea hadi sasa). Badala yake, CBC aliendeleza visasi na uharibifu dhidi ya FBME.

Kinachoshangaza zaidi ni kwamba CBC sasa inataka si tu kusitisha tawi la Cyprus, bali na Benki yenyewe iliyopo Tanzania. Bila shaka kuna sababu nzito hapa, kwa nini baadhi ya viongozi wa CBC wanaridhia kuona mwisho wa FBME, wakidhani hii ndio njia ya kuziba madhambi yao, lakini kakuna kabisa uhalali wa kisheria kwa hatua hii na inaonyesha jinsi gani udhaifu walionao kwenye maamuzi.

**FBME Nchini Cyprus**

Kihistoria, ni muhimu kuzingatia mchango ambao FBME imefanya kwa Cyprus, serikali na watu wake tangu benki ilipoanzishwa hapa mwaka 1982. Tulikuja kisiwani Cyprus kutokea Lebanon na kuwa waanzilishi wa Sekta ya Benki ya Kimataifa nchini na kuvutia benki nyingi za kimataifa kuja kuanzisha biashara hiyo. Kuna wakati ambapo takriban benki 40 za kimataifa na ofisi za wawakilishi zilianzishwa Kisiwani hapa.

Kwa miaka 33 ya mafanikio, FBME imetoa mchango mkubwa sana wa kifedha kwa kulipa mishahara na malipo ya bima ya kijamii, mchango wa kodi, na malipo ya bidhaa za ndani na huduma. Tangu kuanzishwa kwa FBME mwaka 1982, inakadiriwa kuwa thamani yake inafikia EUR milioni 500 na Benki ilikuwa miongoni mwa walipa kodi 20 wakubwa hapa nchini. Kwa kuzungusha kalamu mara moja tu, haya yote yapo hatarini kupotea.

Tumeshiriki katika harakati nyingine za kuiletea maendeleo Cyprus. Kwa mfano wakati wa mdororo wa kifedha ulipoikumba Cyprus kwa mara ya kwanza mwaka 2013, wakati hakukuwa na msaada aliokuja kutoka taasisi nyingine za fedha, za ndani na nje, FBME ilijitosa na kununua hati fungani za muda mrefu za Cyprus ili kujenga

ukwasi uliohitajika wa EUR milioni 240. Kama unavyofahamu, kumekuwa na jaribio la udhalilishaji kwa baadhi ya wanasiasa kuubeza uwekezaji huu. Hata hivyo, ukweli ni kwamba wakati serikali yako inaingia madarakani tuliendelea na uwekezaji huu na tulipunguza hati fungani katika utaratibu makini ambapo ni pale tu ufadhili mbadala ulipokuwepo. Kwa upande wa FBME huu ulikuwa muamala halali kabisa wa kibiashara, na ulipongezwa kwa maandishi na Waziri wa Fedha. Mwaka 2014, Benki ilikuwa ikifikiria utoaji wa ziada wa msaada wa kifedha kwa Jamhuri ya Cyprus chini ya Urais wako, vile vile kuongeza upatikanaji wa fedha za mikopo kwa sekta binafsi ya Cyprus kwa kiasi cha euro milioni 100 ili kusaidia mauzo ya nje. Haya yote yalitoswa majini mwezi Julai 2014!

Kufuatia mlipuko wa Mari, ilikuwa ni FBME tena waliokuja kusaidia kwa kuwekeza EUR milioni 30 kwenye Mamlaka ya Umeme kuisaidia kulipia gharama za urejeshwaji wa umeme uliohitajika sana. Aidha, FBME ni mwanzilishi wa soko la fedha za karatasi za dhamana za serikali ya Cyprus na imesaidia kuzivutia taasisi nyingine. Tunaamini kwamba tuna haki ya kuongelea mafanikio yetu nchini Cyprus kwa njia hii, kwa sababu ya yale tuliyotupiwa kwenye nyuso zetu na kikundi kidogo cha viongozi wa CBC, wanaotaka kifo cha benki yenye ukwasi, kwanza hapa Cyprus na tangu wiki iliyopita nchini Tanzania. Katika hali hii, ni muhimu pia kusema kwamba katika kipindi cha miaka mingi, CBC haijawahi kupata hata muamala mmoja wa fedha chafu, kwa sababu miamala ya aina hiyo haijawahi kuwepo.

**Hatua dhidi ya sheria za kimataifa**

Hatua zilizochukuliwa na CBC dhidi tawi la FBME hazikuzingatia miongozo ya EU, maelekezo na sheria, au sheria za Cyprus. Pia zimeenda kinyume na Mkataba wa Lebanon na Cyprus wa mwaka 2002 juu ya ulinzi wa pamoja wa wawekezaji, makubaliano ambayo CBC wameshindwa kuyaenzi. Jamhuri itahusika kwa hili katika mahakama ya usuluhishi ya ICC mjini Paris, ikifungua milango ya uwezekano wa malipo ya fidia ya mamia ya mamilioni ya Euro. Bila shaka wawekezaji wengine wataweka kwenye kumbukumbu zao kama Serikali za nje zilivyofanya.

Wimbi la kesi za kisheria za kimataifa zinaielemea CBC. Mjini Paris, ICC wamekataa hoja ya Serikali kuhusuiana na uwezo wa mahakama na imeshafikia kwenye hatua ya mwisho. yaani, uchunguzi wa madai ya wamiliki wa FBME. Nchini Marekani, mahakama imeisukuma nyuma FinCEN ili kuchunguza

upya madai yake na ushahidi. Kama unavyojua kutoka kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali wa zamani Bw Alecos Markides kwamba maamuzi ya mwisho ya FinCEN yamesimamishwa na wanatakiwa kufanya mchakato wa kesi upya. Uamuzi mpya wa mwisho unatarajiwa kutolewa na mahakama hiyo katika nusu ya kwanza ya 2016. Kwa maneno mengine, Mheshimiwa Raisi, hatua ya CBC kusitisha leseni ya tawi la FBME imekuja kwa wakati mbaya sana, na kuamsha tuhuma za chinichini kuhusu nia ya viongozi wa CBC. Tunaelewa kwamba hivi ndio jinsi inavyoonekana ndani na nje ya Cyprus. Hatua hii ndio inayoibua maswali mengi kuhusu CBC kuliko majibu. Walati usio muafaka na asili ya mpango na nia ya CBC inaonekana vimetengenezwa ili kutibua utawala wa sheria na utekelezaji wa haki, na haitafanikiwa.

Kuna masuala mengine makubwa kuhusu mwenendo wa CBC na tunayaleta kwako kwa taarifa:

- Nia ya CBC ya kuchukua milki ya tawi la FBME la Cyprus mwezi Julai 2014 inaonekana ni uporaji uliofanywa na CBC dhidi ya maslahi ya wateja na wanahisa na uvunjaji wa wa sheria za Cyprus na za kimataifa
- Jinsi alivyotendewa mdhibiti mkuu wa FBME, Benki Kuu ya Tanzania, kumeshtua wachambuzi wa kimataifa na kwa mara nyingine, mikataba ya kimataifa na MOUs zimevurugwa na CBC kwa vitendo vyake kama vile jaribio la kutaka kuifilisi Benki yote
- Kushindwa kwa CBC kusimamia vizuri Mpango wa Ulinzi wa Amana za Jamhuri (DPS) na jaribio la matumizi haramu ya kutumia fedha za wateja wa FBME kulipia DPS zao wenyewe, ambako kumedhihirika kwa kitendo cha aibu cha CBC kupendekeza mpango huu kwa mdhibiti mkuu.
- Jinsi ilivyotendewa Benki na wanahisa wake kwenye mahakama ya Cyprus, ambayo imesababisha kushindwa kwa mamlaka zote mbili; mahakama na serikali ili kuhakikisha kuwa Benki inatendewa haki katika malengo ya muda mfupi ambayo yamewafaidisha wachache tu;
- Tume zote mbili za makosa ya madai na jinai za CBC, kama vile matumizi mabaya ya fedha za Benki, ambapo kuna ushahidi wa kutosha. Uamuzi wa CBC wa kufuta lseni ya tawi la FBME Cyprus itakuwa ni kigezo binafsi cha Jamhuri kushindwa kwani kutazidisha madhara kwa nchi na walipa kodi wake wakati uamuzi utakapotolewa na mahakama ya ICC mjini Paris. Hii inaweza kuepukwa ikiwa CBC wangekubaliana kujadili kuanzisha njia za kukabiliana na hasara hadi sasa, kama vile kusaidia katika mchakato wa kuhamisha kutoka tawi la Cyprus mali na madeni kwenda Tanzania, ambapo wateja wa FBME wameonyesha kukubali.

Wito kwa Uchunguzi wa Maafisa wa CBC

Haya ni mambo makubwa na yanahitaji uchunguzi makini. Uchunguzi huu ulianzishwa mapema mwaka huu na Baraza la Wawakilishi, ambao mwezi August walitakiwa kuanza kuwahoji viongozi wa CBC juu ya nia yao ya kuisakama FBME. Ni vigumu kuamini katika demokrasia ya kisasa kwani uchunguzi huu uliharibiwa na viongozi wa umma kwa kushirikiana na mabwana zao wa kuchaguliwa, kitendo kisicho cha kidemokrasia ambapo Mwanasheria Mkuu wa Serikali mwenyewe alihusika. Mheshimiwa Rais, nina uhakika utakubaliana nami kwamba hili lina matokeo mabaya sana kwa Jamhuri, wawakilishi wa watu na vyombo vya serikali.

**Nani Anayehusika?**

Wakati tunaitaja CBC hapo juu, hiki ni kikundi kidogo cha Mamlaka ya Azimio, chombo huru cha kisheria ingawa kinaongozwa na uongozi na bodi ya CBC, ambayo hatimaye ndio wanaotoa maamuzi ya hatua hizi. Matokeo ya ukosefu wa mgawanyo wa majukumu kati ya CBC na Mamlaka ya Azimio - napenda urejee kwenye barua ya wazi ya hivi karibuni kwako kutoka kwa mshauri wetu wa sheria, Bw Alecos Markides.Nakuandikia Mheshimiwa Rais kwa kuwa umeweka wazi tamko kwa umma wewe

mwenyewe kuhusu uwezo na uadilifu wa viongozi wa kuteuliwa wa CBC. Kama mlezi wa Jamhuri, msimamo wako katika duru za kimataifa kwa maslahi mapana ya watu wa Cyprus, lazima uwe na wasiwasi na mwenendo wa wale wanaodai kutenda kwa niaba ya nchi. Nina wasiwasi pia kama hoja kutoka FBME zimewasilishwa vizuri kwako.

Mheshimiwa Rais, unatambua ya kwamba tumefanya maombi kadhaa kwa CBC ili kupunguza madhara ya hali inayotukabili sisi sote? Tumeomba kukutana moja kwa moja na kujadili njia ya nje ya msuguano huu na bado narudia wito huo hata katika hatua hii ya mwisho, ili kupata ufumbuzi ambao utakuwa kwa maslahi ya wote wanaohusika. Ufumbuzi huo unaweza kuwa pamoja na:

1. Kuwezesha mchakato wa kuhamisha amana na madeni kutoka tawi la Cyprus kwenda Tanzania.

2. Kusimamisha hatua yoyote ya kibabe ya CBC mpaka matokeo ya kesi ya kimahakama nchini Marekani na ya usuluhishi nchini Ufaransa zimefikia hitimisho. Madhara makubwa yameshafanyika. Tunapaswa kutafuta njia za haraka na zenye ufanisi ili kuhakikisha kwamba hakuna madhara zaidi.

Ayoub-Farid M Saab - Mwenyekiti

CC:
- Rais wa Baraza la Wawakilishi - Yiannakis Omirou
- Kamati ya Maadili ya Bunge
- Benki Kuu ya Ulaya - Mario Draghi
- Tume ya Ulaya - Jean-Claude Juncker
- Averof Neophytou - Mkuu wa DISY
- Andros Kyprianou - Mkuu wa AKEL
- Nicolas Papadopoulos - Mkuu wa DIKO
- Marinos Sizopoulos - Mkuu wa EDEK
- Dimitris Sylouris - Mkuu wa Chama - Ulaya
- George Perdikis - Mkuu wa Chama cha Kijani